# Mkataba Wa Dunia

## UTANGULIZI

Tupo kwenye enzi muhimu katika historia ya Dunia, wakati ambapo binadamu sharti achague mustakabali wake. Pindi ulimwengu unavyozidi kuwa hali ya kutegemeana na dhaifu, siku za usoni zinajipata zikisheheni hatari kubwa na pia ahadi hapo kwa hapo. Ili kuweza kusonga mbele, sharti tutambue kuwa katikati ya mchanganyiko maridhawa wa tamaduni na mifumo ya maisha, sisi ni familia moja ya binadamu na jumuiya moja ya Dunia iliyo na hatima moja. Sharti tujiunge pamoja ili tuanzishe jamii himilifu ya kilimwengu iliyojengwa kwenye misingi ya heshima kwa maumbile, haki za binadamu wote, haki za kiuchumi, na ustaarabu wa kuwa na amani. Ili kufikia hatua hii, ni muhimu kuwa sisi, watu wa Dunia, tutangaze wajibu wetu kwa wenzetu, kwa jumuiya pana ya viumbe, na kwa vizazi vijavyo.

**Dunia, Nyumbani Kwetu**

Binadamu ni sehemu ya ulimwengu mpana unaobadilika. Dunia, nyumbani kwetu, mejaliwa na jumuiya ya kipekee ya viumbe. Misukumo ya kimaumbile hufanya maisha humu duniani kuwa magumu na ya kubahatisha, lakini Dunia imetoa hali ambazo ni muhimu kwa mabadiliko ya maisha. Ukakamavu wa jumuiya ya viumbe na maslahi bora ya binadamu hutegemea utunzaji wa mazingira yenye afya, yakiwa pamoja na mifumo yake yote ya kiekolojia, mchanganyiko mkubwa wa mimea na wanyama, udongo wenye rotuba, maji safi na hewa safi. Mazingira ya kilimwengu pamoja na maliasili yake inayoweza kukadirika ni swala ambalo linawahusu watu wote. Kulinda uhai wa Dunia, pamoja na uchangamano na umaridadi wake ni wajibu mstahifu.

**Hali Ulimwenguni**

Mienendo inayopendelewa ya uzalishaji na utumiaji  inasababisha madhara makubwa kwa mazingira, udumishaji wa maliasili na uangamizaji mkubwa wa baadhi ya viumbe.Jumuiya zinadhoofishwa na hali hii. Manufaa ya maendeleo hayagawanywi kwa usawa ilhali hali nao pengo lililopo baina ya matajiri na maskini linazidi kupanuka. Ukiukaji wa haki, umaskini, ujinga, na matumizi ya mabavu ni mambo ambayo yanasambaa kila mahali na kusababisha mateso makubwa. Ongezeko kubwa kabisa la idadi ya watu limekandamiza mifumo ya kiekolojia na ya kijamii. Misingi ya usalama wa ulimwengu inatishiwa. Mienendo hii ni hatari sana – lakini yaweza kuepukwa.

**Changamoto Zilizo Mbele**

Chaguo ni letu: ama tuunde ushirika wa kilimwengu wa kuitunza Dunia na vile vile kutunzana wenyewe kwa wenyewe, au tuhatarishe kujiangamiza sisi wenyewe na mchanganyiko wa viumbe. Mabadiliko makubwa yanahitajika katika maadili yetu, asasi zetu na njia zetu za maisha. Ni lazima tutambue kuwa baada ya mahitaji ya kimsingi kutimizwa, ustawi wa binadamu kimsingi ni wao kuwa wengi, wala sio kuwa na vingi. Tuna maarifa na teknolojia ya kutimiza mahitaji ya wote na ya kupunguza madhara yetu   kwa mazingira. Kujitokeza kwa jamii ya umma katika utandarithi  kunatoa nafasi mpya za kujenga ulimwengu wenye demokrasia na huruma. Changamoto zetu za kimazingira, kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiroho zimeshikamana pamoja, na kwa pamoja tunaweza kupata masuluhisho yanayoshirikisha watu wote.

**Wajibu wa Watu Wote Ulimwenguni**

Ili kufikia matamanio haya, ni lazima tuamue kuishi kwa moyo wa kuuwajibikia ulimwengu wote, kujitambulisha na jumuiya nzima ya Dunia na hali kadhalika jamii za kikwetu. Sisi tu raia wa mataifa na wakati huo huo wa ulimwengu mmoja ambapo mambo ya kinyumbani na ya kilimwengu yamefungana. Kila mmoja ana sehemu yakeya wajibu kwa maslahi bora ya sasa na ya wakati ujao ya jamii ya kibinadamu na ya ulimwengu mpana wenye viumbe. Moyo wa utangamano wa binadamu na uhusaino baina ya vitu vyote vilivyo hai huimarishwa wakati tunapoishi tukiwa na heshima kubwa kwa fumbo la uhai, kutoa shukrani kwa kipawa cha maisha, na kuwa na unyenyekevu kuhusu nafasi ya binadamu katika maumbile.

Tunahitaji kwa dharura busara ya pamoja kuhusu maadili ya kimsingi ili kutoa nguzo adilifu kwa jumuiya ya ulimwengu inayoibuka. Kwa hiyo, tukiwa pamoja katika matumaini, tunathibitisha kanuni zifuatazo zinazotegemeana ili kuwa na njia himilifu ya maisha kama kigezo cha kawaida ambacho kwacho mwenendo wa watu wote binafsi, mashirika wafanya biashara, serikali, na taasisi za kimataifa zitaelekezwa na kupimwa.

## K A N U N I

## I HESHIMA KWA JUMUIYA YA VIUMBE NA UTUNZAJI WAKE

**1. Heshimu Dunia na viumbe katika uchangamano wake wote.**
a. Tambua kuwa viumbe vyote hutegemeana na kuwa kila aina ya kiumbe ina thamani yake bila kujali manufaa yake kwa binadamu.
b. Thibitisha imani katika hadhi ya kimaumbile ya binadamu wote na katika uwezo wao wa kiakili, kisanaa, kimaadili na kiroho wa binadamu.

**2. Tunza jumuiya ya viumbe kwa upole, huruma na upendo.**
a. Kubali kuwa, pamoja na haki ya kumiliki, kusimamia na kutumia maliasili, hutokea pia na wajibu wa kuzuia uharibifu wa kimazingira na kulinda haki za watu.
b. Thibitisha kuwa pamoja na uhuru, ufahamu na mamlaka yaliyoongezeka, pia huja wajibu ulioongezeka wa kuboresha hali kwa watu wote.

**3. Jenga jamii za kidemokrasia zilizo shirikishi, himilifu, na zenye haki na amani.**
a. Hakikisha kuwa jamii katika viwango vyote zinapata haki za kibinadamu na uhuru wa kimsingi na kumpatia kila mmoja nafasi ya kutumia uwezo wake wote.
b. Kuza haki ya kijamii na kiuchumi itakayowezesha wote kujipatia maisha salama yenye thamani na yanayoiwajibikia ekolojia.

**4. Hifadhi  ukarimu na umaridadi wa Dunia kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.**
a. Tambua kuwa uhuru wa kila kizazi wa kutenda hustahilishwa na mahitaji ya vizazi vijavyo.
b. Pokeza vizazi vijavyo maadili, mila na asasi ambazo huthibiti unawiri wa muda mrefu wa jumuiya za kibinadamu na kiekolojia Duniani.

**Ili kutimiza majukumu haya mapana manne, ni muhimu mambo yafuatayo yatekeleze:**

## II UKAMILIFU WA KIEKOLOJIA

**5. Linda na rudisha ukamilifu wa mifumo ya kiekolojia katika Dunia, hasa kwa kuzingatia zaidi tofauti za kibaolojia na mifanyiko ya kimaumbile inayothibiti uhai.**
a. Tumia katika viwango vyote, mipango na kanuni za maendeleo himilifu ambayo yatafanya uhifadhi na ukarabati wa mazingira kuwa jambo muhimu katika shughuli zote za maendeleo.
b. Anzisha na pia linda hifadhi za kimaumbile zilizo na uwezo wa kuzalisha, zikiwa ni pamoja na mbuga na sehemu za majini, ili kulinda mifumo ambayo huthibiti maisha katika Dunia, kudumisha bayoanuwai, na kuhifadhi turadhi zetu za asilia.
c. Hamasisha uhuishaji wa viumbe na mifumo-ekolojia iliyohatarisha.
d. Thibiti na angamiza viumbe visivyo asilia ama vile vya kinasaba ambavyo hudhuru viumbe asilia na mazingira, na pia zuia uanzishwaji  wa viumbe hivi vyenye madhara.
e. Simamia  matumizi ya maliasili zinazoweza kurudiwa  tena kama vile maji, udongo, bidhaa za miti, na viumbe vya majini kwa njia ambazo hazikiuki viwango vya kurudiwatena ama kuzaana tena na ambazo hulinda afya ya mifumo ya kiekolojia.
f. Simamia uchimbaji na matumizi ya maliasili ambazo hazirudiwi tena kama vile madini na mafuta yatokanayo na viumbe waliokufa zamani, kwa njia ambazo hazitasababisha kuisha kwake na ambazo hazileti madhara makali kwa mazingira.

**6. Zuia uharibifu kama njia bora zaidi ya kulinda mazingira, na wakati hakuna maarifa ya kutosha, tumia mkabala wa tahadhari.**

a. Chukua hatua za kuzuia uwezekano wa kutokea kwa madhara mabaya au yasiyorekebishika kwa mazingira hata wakati maarifa ya kisayansi hayajakamilika wala kuhitimika.
b. Wekea jukumu la kudhihirisha ukweli kwa wanaodai kuwa vitendo au shughuli ambazo wanapendekeza kufanya hazitasababisha madhara makubwa na wafanye wale wanaohusika walipie uharibifu utokeao kwa mazingira.
c. Hakikisha kuwa utoaji maamuzi unazingatia matokeo limbikizi, ya muda mrefu, yasiyo ya moja kwa moja, ya mbali na ya kilimwengu juu ya shughuli za binadamu.
d. Zuia uchafuzi wa sehemu yoyote ya mazingira na usiruhusu kurundikana kwa miale na kemikali za sumu ama zile zinazoweza kuleta madhara ya kiafya na kimazingira.
e. Epusha shughuli za kijeshi zinazoleta uharibifu kwa mazingira.

**7. Tumia ruwaza za uzalishaji, utumizi na uzalishaji tena ambazo hulinda uwezo wa Dunia wa kuzalisha tena, haki za kibinadamu na hali bora ya maisha katika jamii.**
a. Punguza, tumia tena na rudia tena malighafi itumiwayo katika mifumo ya uzalishaji na utumizi, na hakikisha kuwa mabaki ya takataka yanaweza kumezwa na mifumo iliyoko ya kiekolojia.
b. Kuwa na tahadhari, na makini wakati wa kutumia kawi, na tegemea kwa kiwango kikubwa kawi inayoweza kurudiwa tena kama vile jua na upepo.
c. Himiza, ustawishaji, matumizi, na uhamishaji sawia wa teknolojia zinazopendelea mazingira bora.
d. Jumuisha gharama kamili za kimazingira na kijamii za bidhaa na huduma kwenye bei yake, na uwawezeshe watumiaji watambue bidhaa ambazo zinaafikia viwango vya juu zaidi vya kijamii na kimazingira.
e. Hakikisha kwamba watu wote wanapata huduma za afya ambazo huimarisha afya ya uzazi na uzazi unaofaa.
f. Chukua mienendo ya maisha ambayo husisitiza ubora wa afya na utoshelezaji wa mali katika ulimwengu ulio na mwisho.

**8. Pevusha masomo ya udumishaji wa ekolojia na himiza ubadilishani wazi na matumizi mapana ya maarifa yapatikanayo.**
a. Unga mkono ushirikiano na kimataifa wa kisayansi na kiufundi kuhusu udumishaji, huku ukiyapa umbele mahitaji ya mataifa yanayostawi.
b. Tambua na hifadhi maarifa ya kimila, na hekima ya kiroho katika tamaduni zote ambazo huchangia katika utunzaji wa mazingira na maslahi bora ya binadamu.
c. Hakikisha kuwa habari muhimu sana kwa afya ya binadamu na kwa utunzaji wa mazingira, ikiwa ni pamoja na habari juu ya maumbile ya kijeni, zinapatikana katika himaya ya umma.

## III. HAKI ZA KIJAMII NA KIUCHUMI

**9. Angamiza umaskini kama jukumu la kimaadili, kijamii na kimazingira.**
a. Hakikisha haki ya kuwa na maji safi, hewa safi, usalama wa chakula, udongo usiochafuliwa, maskani, na misala salama, na pia gawa raslimali za kitaifa na kimataifa zinazohitajika.
b. Kabidhi kila binadamu uwezo wa kielimu na mali ya muwezeshe apate maisha himilifu, na hakikisha usalama wa kijamii pamoja na kutoa hifadhi kwa wale ambao hawawezi kujisimamia.
c. Tambua waliopuuzwa, linda wale walio wanyonge, hudumia wale wanaoteseka na wawezeshe kukuza uwezo wao na kutafuta matamanio yao.

**10. Hakikisha kuwa shughuli na asasi zote za kiuchumi katika viwango vyote zinachochea maendeleo ya kibinadamu kwa njia ya sawia na himilifu**
a. Kuza ugawaji sawia wa mali ndani ya mataifa na baina ya mataifa.
b. Zidisha raslimali za kitaaluma, kifedha, kiufundi na kijamii za mataifa yanayostawi, na pia yaondolewe madeni mazito ya kimataifa.
c. Hakikisha kuwa biashara zote zinaunga mkono matumizi dumishi ya raslimali, uhifadhi wa mazingira, na ustawi wa viwango bora vya utendaji kazi.
d. Sisitiza kuwa makampuni makubwa na mashirika ya kimataifa ya kifedha yanatekeleza wajibu wao kwa uwazi kwa manufaa ya umma, na pia yafanye yawajibikie matokeo ya shughuli zao.

**11. Imarisha usawa na usawia wa kijinsia kama hitaji la maendeleo himilifu na hakikisha kuwa elimu, huduma za matibabu na nafasi za kiuchumi zinafikiwa na watu wote ulimwenguni.**

a. Linda haki za kibinadamu za wanawake na wasichana na pia maliza dhuluma zote dhidi yao.
b. Endeleza ushiriki kamili wa wanawake katika shuguli zote za maisha ya kiuchumi, kisiasa, kiraia, kijamii, na kitamaduni wakiwa washirika kamili na sawa, watoa-maamuzi, viongozi, na wafaidi.
c. Imarisha familia na hakikisha kuna usalama na malezi yenye upendo kwa watu wote katika familia.

**12. Linda haki za wote, bila ubaguzi, kwa mazingira asilia na ya kijamii yanayohimili hadhi ya binadamu, afya ya mwili, na hali bora ya kiroho, hasa kwa kuzingatia haki za jamii za wenyeji na walio wachache.**
a. Maliza aina zote za ubaguzi, kama vile ubaguzi wa rangi, kabila, uana, mwelekeo wa kimapenzi, dini, lugha, na ule utokanao na asili ya kitaifa, kikabila na kijamii.
b. Sisitiza haki ya jamii za wenyeji ya kuwa ha hali yao ya maisha ya kiroho, maarifa, ardhi na raslimali na pia kwa mbinu zao za kuishi maisha himilifu.
c. Heshimu na unga mkono vijana wa jamii zetu, wawezeshe watimize wajibu wao muhimu katika kuunda jamii himilifu.
d. Linda na rudisha sehemu maarufu zilizo na umuhimu wa kitamaduni na kiroho.

## IV. DEMOKRASIA, AMANI NA KUTOTUMIA MABAVU

**13. Imarisha asasi za kidemokrasia katika viwango vyote, na onyesha uwazi na uwajibikaji katika utawala, ushirikishaji katika utoaji wa maamuzi, na upataji wa haki.**
a. Linda haki ya kila mtu ya kupokea habari kamilifu na kuwa wakati ufaao, kuhusu maswala ya kimazingira pamoja na za mipango na shughuli zote za kimaendeleo ambazo zaweza kuwaathiri au zile zinazowahusu.
b. Unga mkono jamii za umma wa jumuiya, maeneo na ulimwengu na himiza kushiriki kwa watu wote binafsi na mashirika husika katika utoaji wa maamuzi.
c. Linda haki za kuwa na uhuru wa kutoa maoni, kujieleza, kutangamana kwa amani, kujishirikisha pamoja, na kutokubaliana.
d. Anzisha njia muafaka na madhubuti ya kufikia taratibu za utawala na mahakama huru pamoja na zile za kurekebisha na kufidia kwa madhara ya kimazingira na pia tishio la madhara kama hayo.
e. Maliza ufisadi katika asasi zote za umma na za kibinafsi.
f. Imarisha jumuiya za mitaa, kwa kuziwezesha kutunza mazingira yao na pia toa majukumu ya kimazingira kwa ngazi za serikali ambako yanaweza kutekelezwa ipasavyo.

**14. Jumuisha kwenye mfumo rasmi wa elimu na katika mafunzo ya maisha yote, maarifa, maadili, na ujuzi unaohitajika katika maisha himilifu.**
a. Wape watu wote, hasa watoto na vijana, nafasi za kielimu ambazo zitawapa uwezo wa kuchangia kikamilifu katika maendeleo himilifu.
b. Endeleza mchango wa masomo ya sanaa na utamaduni na pia yale ya sayansi kwenye elimu himilifu.
c. Kuza wajibu wa vyombo vya habari katika kutoa ufahamu wa changamoto za kiekolojia na za kijamii.
d. Tambua umuhimu wa elimu ya kimaadili na ya kiroho kwa maisha himilifu.

**15. Shughulikia viumbe vyote vyenye uhai kwa heshima na huruma.**
a. Zuia ukatili kwa wanyama wanaofugwa katika jamii za kibinadamu na walinde kutokana na mateso.
b. Linda wanyama wa pori kutokana na mbinu za uwindaji, utegaji, na uvuvi ambazo husababisha mateso makali, ya muda mrefu au yanayoweza kuzuiliwa.
c. Epuka au maliza kadri iwezekanavyo uhasiri au uangamizaji wa viumbe ambavyo havikuwa vimelengwa.

**16. Endeleza ustaarabu wa kuvumiliana, kutotumia mabavu, na kuwa na amani.**
a. Himiza na uunge mkono maridhiano baina ya mmoja na mwingine, mshikamano, na ushirikiano baina ya watu wote katika taifa na baina ya mataifa.
b. Tekeleza mikakati madhubuti ya kuzuia makabiliano makali na tumia usuluhishaji shirikishi wa matatizo katika kuthibiti na kusuluhisha mizozo ya kimazingira na mingineyo.
c. Ondoa wanajeshi kutoka kwa mifumo ya usalama wa kitaifa hadi kufikia kiwango cha kujitetea, na geuza raslimali za kijeshi kwa matumizi ya kuleta amani, ikiwa ni pamoja na uhuishaji wa ekolojia.
d. Angamiza zana za kinuklia, za sumu, za kibiolojia na zile ziletazo maafa makubwa.
e. Hakikisha kuwa matumizi ya mzingo na anga za juu huunga mkono ulinzi wa mazingira na amani.

f. Tambua kuwa amani ni ukamilifu uletwao na mahusiano yafaayo kwa mtu mwenyewe binafsi, baina yake na watu wengine, tamaduni zingine, uhai mwingine, Dunia, na pia ule ukamilifu mpana ambao vyote si sehemu yake.

## MIKAKATI YA SIKU ZA USONI

Kama ambavyo haijapata kutokea katika historia, hatima ile ya pamoja inatuhimiza tutafute mwanzo mpya. Mwanzo huu ndio ahadi ya kanuni hizi za hati ya Makataba wa Dunia. Ili kutimiza ahadi hii, ni sharti tujitolee kuchukua na kukuza maadili na malengo ya Mkataba huu.

Hii huhitaji mabadiliko ya mawazo na ya moyo. Inahitaji moyo mpya wa utegemeanaji wa kilimwengu na wajibu wa wote ulimwenguni. Ni sharti kimawazo tuanzishe na tutekeleze busara ya hali himilifu ya maisha kijijini, kitaifa, kieneo, na kilimwengu. Mchanganyiko wetu wa kitamaduni ni turadhi yenye thamani na tamaduni tofauti zitatafuta njia zao za kipekee za kufikia busara hii. Ni sharti tuongeze kina na tupanue mjadala wa kilimwengu ulioibusha Makataba wa Dunia, kwa kuwa tuna mengi ya kujifunza kutokana na harakati shirikishi na zinazoendelea za kutafuta ukweli na hekima.

Maisha aghalabu huhusu mivutano baina ya maadili muhimu. Hali hii humaanisha uteuzi mgumu. Hata hivyo, ni sharti tutafue njia za kuoanisha uchangamano na umoja, utekelezaji wa haki ya uhuru kwa manufaa ya wote, malengo ya muda mfupi na shabaha ya muda mrefu. Kila mtu, familia, shirika, na jumuiya ina wajibu muhimu wa kutekeleza.
Sanaa, sayansi, dini, vyuo vya elimu, vyombo vya habari, biashara, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, na serikali vyote vyaombwa vitoe uongozi bunifu. Ushirika wa serikali, jumuiya ya umma, na kufanya biashara ni muhimu kwa utawala bora.

Ili kujenga jumuiya himilifu ya kilimwengu, mataifa ya dunia sharti yaanzishe upya wajibu wao kwa Umoja wa Mataifa, yatimize majukumu yao chini ya mikataba iliyoko ya kimataifa, na yaunge mkono utekelezwaji wa kanuni za hati ya Mkataba wa Dunia kwa kutumia chombo cha kimataifa chenye makubaliano ya kisheria juu ya mazingira na maendeleo.

Hebu wakati wetu ukumbukwe kuwa ule wa kuzindua ustahifu mpya kwa maisha, azma thabiti ya kufikia uhimilifu, kuharakishwa kwa harakati za kupigania haki na amani, pamoja na kusherehekea maisha kwa furaha.